



KAUNTI YA ERIE

MARK POLONCARZ

MKUU WA KAUNTI

GALE R. BURSTEIN, MD, MPH, FAAP
KAMISHNA WA AFYA

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU KUTENGWA KUTOKANA NA COVID-19

Je, hii inamhusu nani?

Mtu yeyote anayekaa katika Kaunti ya Erie, ambaye ana COVID-19

Je, nimetengwa?

Mkazi yeyote wa Kaunti ya Erie ambaye ana COVID-19 atatengwa kwa mujibu wa Utaratibu Mkuu wa Kamishna.

Je, ni nini kitakachotendeka nikipuuzwa agizo la kutengwa?

Kupuuzwa agizo la kutengwa ni kosa linaloadhibiwa kwa mujibu wa Sehemu ya 12-b ya Sheria ya Afya ya Umma. Vilevile, Idara ya Afya inaweza kuomba kukufungia katika kituo cha afya kwa kukosa kutii.

Sawa, ninaweza kujiondoa vipi katika sehemu niliyotengwa?

Lazima usalie sehemu uliyotengwa hadi utimize Vigezo vya Uthibitishaji vilivyowekwa na Idara ya Afya ya Jimbo la New York. Pindi tu unapotimiza Vigezo vya Uthibitishaji, unaweza kuondoka sehemu uliyotengwa.

Je, Vigezo vya Uthibitishaji ni vipi?

Hivi hapa Vigezo:

Ikiwa umeonyesha dalili yoyote kati ya zifuatazo: Joto jingi, Kikohozi, Kuhema/Ugumu wa Kupumua, Vigezo vya Uthibitishaji ni:

- Zimekuwa angalau siku 7 tangu ulipoanza kuonyesha dalili mara ya kwanza; NA
- Hujawa na joto jingi kwa angalau siku 5, bila kumeza dawa za kupunguza joto jingi (kama vile Tylenol); NA
- Kuhema/kukohoa/ugumu wa kupumua wowote umeimarika.

Ukitimiza vigezo VYOTE VITATU, unaweza kuondoka kwenye sehemu uliyotengwa.

Ikiwa hujaonyesha dalili yoyote kati ya hizo, Vigezo vya Uthibitishaji ni:

- Zimekuwa angalau siku 7 tangu ulipofanyiwa kipimo cha kuwa na COVID-19 mara ya kwanza; NA
- Hujawa na ugonjwa wowote baadaye

Ukitimiza vigezo VYOTE VIWILI, unaweza kuondoka kwenye sehemu uliyotengwa

Kwa hivyo nikitimiza Vigezo vya Uthibitishaji niko huru kabisa?

LA! Kutimiza Vigezo vya Uthibitishaji kunakuweka huru tu kutoka kwenye sehemu ya matibabu uliyotengwa. Bado unapaswa kufuata Sheria nyingine zote za Jimbo na Serikali ya Mitaa zinazotumika na Amri za Rais. Kwa mfano:

MAMBO UNAYOWEZA KUFANYA	MAMBO USIYOWEZA KUFANYA
Kuenda kwenye duka la mboga na matunda	Kuenda kwenye sherehe
Kuenda kutembea nje	Kucheza michezo na kikundi cha watu
Kuenda kazini ikiwa unafanya kazi ya biashara inayotoa huduma muhimu kama ilivyobainishwa na Empire State Development Corporation	Kuenda kazini ikiwa hufanyi kazi ya biashara au huduma muhimu.

Je, kuna maagizo mengine yoyote maalum ninayopaswa kufahamu?

Ikiwa wewe ni mhadumu wa afya, mhadumu wa dharura, au mfanyakazi mwingine muhimu anayerejea kufanya kazi unahitajika kuvaa barakoa kwa siku 14 baada ya mwanzo wa ugonjwa au baada ya kupatikana na COVID-19 bila kujali uwepo wa dalili. Tafadhali wasiliana na mwajiri wako kwa maagizo yoyote ya ziada.

Lakini ikiwa nimethibitishwa kutokuwa na virusi, siwezi kumfanya mtu mwingine yeyote kuwa mgonjwa, sivyo?

Si sahihi. Ingawa Vigezo vya Uthibitishaji vimeundwa ili kupunguza hatari ya kusambaa kwa COVID-19, bado unaweza kuwaambukiza watu wengine.

Ninaweza kufanya nini ili kuepuka hali hiyo?

Kuwa makini. Nawa mikono yako vizuri sana na mara kwa mara. Funika mdomo unapokohoa. Epuka kukaa karibu na yeyote aliye na zaidi ya miaka 65 au yeyote aliye na mfumo wa kingamaradhi ulioathirika au ugonjwa kabla ya korona. Dumisha kukaa mbali na watu. Kaa nyumbani isipokuwa uwe na haja ya kuenda nje.

Ninaelewa yote hayo. Je, ninahitaji chochote kutoka kwenye Idara ya Afya?

Hapana. Pindi tu unapotimiza Vigezo vya Uthibitishaji, kipindi chako cha kujitenga kinaisha.